

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 2322761-5
Fax No. +255 026 2324218
E-mail: cna@bunge.go.tz



Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole
S.L.P. 941,
41105 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Kamati nne za Kudumu za Bunge zinawaalika wadau kutoa maoni kuhusu Miswada minne ya Sheria iliyosomwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge. Vikao vyote vya kupokea maoni ya Wadau vitafanyika siku ya Jumatano tarehe 19 Oktoba, 2022 kuanzia saa 3.00 Asubuhi.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira itapokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 2022. Kikao cha kupokea maoni hayo kitafanyika katika Ukumbi: Na. 49, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex).

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria itapokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 wa Mwaka 2022. Kikao cha kupokea maoni hayo kitafanyika katika Ukumbi: Na. 9 Jengo Kuu la Utawala.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii itapokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Kikao cha kupokea maoni hayo kitafanyika katika Ukumbi wa Spika, Jengo la Pius Msekwa.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu itapokea maoni ya Wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2022. Kikao cha kupokea maoni hayo kitafanyika katika Ukumbi: Na. 38, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex). Miswada yote inaweza kupakuliwa katika tovuti ya Bunge ambayo ni www.bunge.go.tz

Aidha, Kamati zitapokea maoni kwa njia ya posta au kwa barua pepe kwa anuani ifuatayo: -

Katibu wa Bunge,
Ofisi ya Bunge,
Mtaa wa Makole,
S. L. P. 941,
41105 DODOMA.

Baruapepe: cna@bunge.go.tz na kamati@bunge.go.tz

Imetolewa na:- Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

07 Oktoba, 2022.